TANGAZO LA SERIKALI NA. 498 la tarehe 15/7/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

SHERIA NDOGO

(Imetungwa chini ya vifungu vya 6 (1) na 16(1))

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO YA MWAKA 2022

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ya Mwaka 2022.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

SEHEMU YA PILI

UTOZAJI ADA NA USHURU

Utozaji wa ada na ushuru

3.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

5.- (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

6.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

(6) Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa au Wakala hataruhusiwa kukamata au kuuza bidhaa au mali iliyokamatwa bila kupata idhini ya

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

Afisa Masuuli.

Uteuzi wa Wakala

7. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Mamlaka ya Afisa Mwidhini wa

8. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

SEHEMU YA TATU
MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

9.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru; na

e) akishindwa kuweka kumbukumbu za vitabu, hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha kwanza atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Tangazo la Selikali Na. 225 la Mwaka 2019

11. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, 2019.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 3(1))

SEHEMU YA KWANZA

Ushuru wa kukodisha mali za Halmashauri

Na.	**Aina ya chanzo**	**Kiasi cha ushuru/Ada**	**Muda**
1.	Catapillar	i. 800,000/= kwa taasisi za kibiashara/serikali /makampuni.	Saa nane.
		ii. 400,000/= kwa wananchi wa kawaida.	Saa nane.

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

SEHEMU YA PILI

Ada ya usajili wa uchimbaji wa madini na usafirishaji wa madini kwa uzito

Na.	Chanzo	Kiasi	Muda/Kipimo
i	Usajili wa umiliki wa madini ya mchanga na kifusi	300,000/=	Mwaka
ii	Usajili wa Umiliki wa madini ya kokoto,moramu na chokaa	300,000/=	Mwaka
iii	Usafirishaji madini kwa uzito chini ya tani 7	3000/=	Kwa tripu
iv	Usafirishaji madini kwa uzito wa tani 8-10	5000/=	Kwa tripu
v	Usafirishaji madini kwa uzito zaidi ya tani 10	10,000/=	Kwa tripu

SEHEMU YA TATU

Ada ya Kupima Afya

Na.	Aina ya chanzo	Kiasi	Muda
1.	Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa migahawa na saloon.	5,000/=	Mwaka.
2.	Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa kwenye bar.	10,000/=	Mwaka
3.	Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa hotel na	30,000/=	Mwaka

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

	viwandani		

SEHEMU YA NNE

Ada ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi

(A)	MAKAZI KUWA BIASHARA	
	1. Makazi ya Familia Zaidi ya Moja	100,000/=
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000/=
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 6	200,000/=
	c) Makazi ya Familia 7 hadi 8	300,000/=
	d) Zaidi ya 10	200,000/=
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	50,000/=
	3. Ofisi	400,000/=
	4. Huduma	400,000/=
	5. Karakana(Service trade)	400,000/=
	6. Viwanda	250,000/=
	7. Makazi Biashara na Ofisi	
	8. BIASHARA:	250,000/=
	a) Mgahawa	300,000/=
	b) Nyumba ya kulala wageni	700,000/=
	c) Hoteli	700,000/=
	d) Maduka makubwa(Super market)	1,000,000/=
	e) Kituo cha mafuta	500,000/=
	f) Kumbi	500,000/=
	g) Baa	

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

(B)	KARAKANA(SERVICE TRADE)	
	1. Makazi ya Familia Zaidi ya Moja	
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000/=
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 6	300,000/=
	c) Makazi ya Familia 7 hadi 8	300,000/=
	d) Zaidi ya 10	400,000/=
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	300,000/=
	3. Ofisi	200,000/=
	4. Huduma	100,000/=
	5. Viwanda	1,000,000/=
	6. Makazi Biashara na Ofisi	300,000/=
	8. BIASHARA:	
	a) Mgahawa	200,000/=
	b) Nyumba ya kulala wageni	300,000/=
	c) Hoteli	700,000/=
	d) Maduka makubwa(Super	700,000/=
	market)	1,000,000/=
	e) Kituo cha mafuta	500,000/=
	f) Kumbi	500,000/=
	g) Baa	
(C)	HUDUMA	
	1. Makazi ya Familia Zaidi ya Moja	
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	500,000/=
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 6	700,000/=
	c) Makazi ya Familia 7 hadi 8	800,000/=
	d) Makazi ya Familia 9 hadi 10	1,000,000/=
	d) Zaidi ya 10	1,200,000/=
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	700,000/=
	3. Ofisi	500,000/=

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

	5. Karakana(Service trade)	1,000,000/=
	6. Viwanda	1,000,000/=
	7. Makazi Biashara na Ofisi	700,000/=
	8. BIASHARA:	
	a) Mgahawa	800,000/=
	b) Nyumba ya kulala wageni	850,000/=
	c) Hoteli	1,000,000/=
	d) Maduka makubwa(Super market)	1,000,000/=
	e) Kituo cha mafuta	1,000,000/=
	f) Kumbi	1,000,000/=
	g) Baa	
(D)	MAKAZI PEKEE	
	1. Makazi ya Familia Zaidi ya Moja	
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000/=
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 10	300,000/=
	c) Zaidi ya 10	500,000/=
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	300,000/=
	3. Ofisi	400,000/=
	4. Huduma	100,000/=
	5. Karakana(Service trade)	500,000/=
	6. Viwanda	500,000/=
	7. Makazi Biashara na Ofisi	400,000/=
	8. BIASHARA:	
	a) Mgahawa	300,000/=
	b) Nyumba ya kulala wageni	400,000/=
	c) Hoteli	1,000,000/=
	d) Maduka makubwa(Super	1,000,000/=

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

	market)	1,000,000/=
	e) Kituo cha mafuta	1,000,000/=
	f) Kumbi	1,000,000/=
	g) Baa	
(E)	OFISI	
	1. Makazi ya Familia Zaidi ya Moja	
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000/=
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 10	300,000/=
	c) Zaidi ya 10	500,000/=
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	300,000/=
	3. Huduma	100,000/=
	4. Karakana(Service trade)	500,000/=
	5. Viwanda	500,000/=
	6. Makazi Biashara na Ofisi	500,000/=
	8. BIASHARA:	300,000/=
	a) Mgahawa	300,000/=
	b) Nyumba ya kulala wageni	1,000,000/=
	c) Hoteli	1,000,000/=
	d) Maduka makubwa(Super	1,000,000/=
	market)	1,000,000/=
	e) Kituo cha mafuta	1,000,000/=
	f) Kumbi	1,000,000/=
	g) Baa	
(F)	VIWANDA	
	1. Makazi ya Familia Zaidi ya Moja	
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000/=
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 10	300,000/=
	c) Zaidi ya 10	500,000/=

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

	2. Makazi na Biashara ya Maduka 3. Ofisi 4. Huduma 5. Karakana(Service trade) 6. Makazi Biashara na Ofisi 8. BIASHARA: a) Mgahawa b) Nyumba ya kulala wageni c) Hoteli d) Maduka makubwa(Super market) e) Kituo cha mafuta f) Kumbi g) Baa	300,000/= 400,000/= 100,000/= 500,000/= 500,000/= 300,000/= 300,000/= 1,000,000/= 1,000,000/= 1,000,000/= 1,000,000/= 1,000,000/=
(G)	NYONGEZA YA SAKAFU Ada italipwa kwa kuzingatia eneo la mraba (square. metre) la sakafu ya jengo iliyoongezeka.	60,000/= hadi 1,200,000/=
(H)	Marekebisho ya mchoro wa Mipango Miji	100,000
(I)	Michoro mipya	50,000
(J)	Utumiaji wa maeneo ya wazi (Open Spaces)	15,552/= kwa mita za mraba (maeneo ya Mjini) 7,776/= kwa mita za mraba (maeneo ya Pembezoni mwa Mji)

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

SEHEMU YA TANO

Ada na Vibali mbalimbali

(a)	Ada ya fomu za maombi ya zabuni (Kitaifa) Ada ya fomu za maombi ya zabuni (Kimataifa)	100,000/= 300,000/=	
(b)	Kibali cha kuweka kontena la biashara	Kontena la futi 40	500,000/= kwa mwaka
		Kontena la futi 20	250,000/= kwa mwaka
(c)	Kibali cha kuweka kioski	200,000/=	
(d)	Kibali cha Upimaji	100,000/=	
(e)	Huduma ya Kupima Ardhi kwa kila kiwanja kilichopimwa kwa Makampuni Binafsi	100,000/=	
(f)	Ada ya Vibali vya Ujenzi		
	Eneo linalozidi (Built up Area) (Mita za Mraba).	Eneo Lisilozidi (Built up Area) (Mita za Mraba).	
		49.45	60,000.00
	49.45	92.90	80,000.00
	92.90	139.35	120,000.00
	139.35	185.8	148,000.00
	185.8	278.7	180,000.00
	278.7	371.6	300,000.00
	371.6	464.5	360,000.00
	464.5	557.4	440,000.00
	557.4	650.3	480,000.00
	650.3	929	1,200,000.00
		Ada kwa kila 92.90m^2 itakayoongezeka	30,000.00

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

(g)	Kibali cha Ujenzi wa Vituo vya Mafuta.	1,200,000/=
(h)	Kibali cha Ujenzi wa Mnara	300,000/=
(i)	Kibali cha Ukarabati Mdogo	100,000/=
(j)	Ada ya Maombi ya Viwanja	50,000/=
(k)	Nukuu ya bei (Quotation) kwa kila fomu	50,000/=
(l)	Kibali cha uzio	
	a. Eneo dogo(High Density)	100,000/=
	b. Eneo la Kati(Medium Density)	150,000/=
	c. Eneo Kubwa(Low Density)	300,000/=
	d. Eneo Kubwa lililozidi(Super Low Density)	500,000/=
(m)	Kibali cha kuzungusha mabati (hoarding).	5000/= hadi 10000/= kwa urefu futi moja(per running feet)
(n)	Kibali cha kubomoa	
	a. Eneo dogo(High Density)	100,000/=
	b. Eneo la Kati (Medium Density)	150,000/=
	c. Eneo Kubwa(Low Density) na kuendelea	300,000/=
	d. Eneo Kubwa lililozidi(Super Low Density)	500,000/=
	e. Mnara wa simu	300,000/=

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

SEHEMU YA SITA

Ushuru wa Mazao ya Maliasili

1	Duka la mbao	51,000/=
2	Duka la mkaa	51,000/=
3	Duka la Kuni	51,000/=
4	Kiwanda cha samani(funiture)	51,000/=
5	Nguzo	51,000/=
6	Magogo	51,000/=
7	Vinyago	51,000/=
8	Duka la Miti	51,000/=
9	Yadi ya Mbao	51,000/=
10	Fito	51,000/=
11	Gunia la mkaa (mfuko wa kg 25)	500/=
12	Gunia la mkaa (mfuko wa kg 100)	1,000/=
13	Viwanda vya mbao (woodworks factory) vyenye ukubwa wa kuchakata mbao chini ya 5,000m3 kwa mwaka	102,000/=

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

14	Viwanda vya mbao (woodworks factory) vyenye ukubwa wa kuchakata mbao zaidi ya 5,000m3 kwa mwaka	200,000/=
15	Kukata miti ya hifadhi kupisha ujenzi(maendelezo)	50,000/=
16	Lori la Mkaa zaidi ya 2.5 Tani	10,000/=
17	Lori la Mbao zaidi ya 2.5 Tani	10,000/=
18	Kibali cha kukata miti/kupunguza matawi (Cubic Meter) (CM^3)	5,000/=
19	Kibali cha kufuga Wanyama Pori wa miguu minne	50,000/=
20	Kibali cha kufuga Wanyama Pori wengine	20,000/=

SEHEMU YA SABA

Ada ya kuendesha shughuli za Utamaduni, Burudani na Michezo

1	Tamasha lenye hadhi ya Kitaifa	200,000/=	Kwa tukio moja
2	Tamasha lenye hadhi ya Kimkoa	100,000/=	Kwa tukio moja
3	Tamasha lenye hadhi ya Kiwilaya	50,000/=	Kwa tukio moja
4	Tamasha lenye hadhi ya Kata	30,000/=	Kwa tukio moja
5	Tamasha lenye hadhi ya Mtaa	20,000/=	Kwa tukio moja
6	Waombaji wa kibali cha burudani ndani ya ukumbi	10%	Gharama ya ukumbi

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

7	Matangazo kwa kutumia vyombo (promosheni)	50,000/=	Kwa tukio moja

SEHEMU YA NANE

Ushuru wa Kushusha na kupakia mizigo

Gari zaidi ya tani mbili hadi tani 3.5

- Tshs. 15,000 kwa siku
- Ths. 100,000 kwa mwezi mmoja.

Gari zaidi ya tani 3.5 hadi tani 10

- Tshs. 30,000 kwa siku moja
- Ths. 150,000 kwa mwezi mmoja

Gari zaidi ya tani 10

- Tshs. 100,000 kwa siku moja
- Ths. 500,000 kwa mwezi mmoja

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

SEHEMU YA TISA

Ada ya Usajili wa Magari ya Biashara kwa Mwaka

Na.	Aina ya Gari	Kiwango cha Ada	Muda
1.	Taksii	40,000/=	Mwaka
2.	Gari ya mizigo(Pick Up) chini ya tani 3	60,000/=	Mwaka
3.	Lori tani 3.5 hadi tani 7	80,000/=	Mwaka
4.	Lori tani 7 na kuendelea	100,000/=	Mwaka
5.	Gari lolote la mizigo chini ya tani 1	30,000/=	Mwaka
6.	Gari dogo la abiria	50,000/=	Mwaka
7.	Gari kubwa la abiria	180,000/=	Mwaka
8.	Gari lolote dogo la biashara lisilotajwa hapo juu.	50,000/=	Mwaka
9.	Gari lolote kubwa la biashara lisilotajwa hapo juu.	100,000/=	Mwaka
10.	Vyombo vya moto vya magurudumu mawili na matatu	36,000/=	Mwaka.

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 10)

Mimi ……. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……. ambaye ni Mkurugenzi Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi…….. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za(Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za mwaka, 2022.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe ……..ya Mwezi …… Mwaka ……

Jina: …….Saini: …….

Mbele ya:

Jina: ……Cheo: …….

Saini: ……..

Tarehe: ……

Tangazo la Serikali Na.. 498 (linaendelea)

Nembo na Mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea imebandikwa kwenye Sharia ndogo hizi kufutia Azimio liliilopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Mdiwani uliofanyika mnamo tarehe 13 Mwezi Agosti,2022

BEATRICE R DOMINIC,
Mkurugenzi wa,
Halmashauri ya Manispaa
Ubungo

JAFFARY JUMA NYAIGESHA
Mstahiki Meya,
Halmashauri ya Manispaa
Ubungo

L.S

NAKUBALI

Dodoma,
29 Juni,2022

INNOCENT BASHUNGWA (MB),
Waziri wa Nchi-OR-Tamisemi